

Angizo La Afisa Wa Afya Wa Mtaa Wa Kaunti Ya King

Maski zinahitajika kwa sasa kwa ukumbi
wowote wa ndani ulio na watu 500 au zaidi
waliohudhuria.

Hili angizo ni la wote wale waliopata na hawajaopata chanjo,
umri wa miaka 5 na zaidi.



Maski pia zinapendekezwa sana kwa sasa kwa watu wote wenye umri wa miaka 5 na zaidi — wote waliopata na wale hawajapata chanjo — kwenye hali yoyote ingine ya nje ambapo watu hawawezi kukaa angalau fiti 6 mbali na mtu ambaye si mkazi wa nyumbani humo.



← chini ya fiti 6 →



Kwa nini angizo mpya la maski nje?

- Kaunti ya King ina viwango za juu vinavyozidi kuongezeka za uambukizaji wa COVID-19.
- Mfumo wetu wa huduma wa afya upo katika changamoto kubwa sana.
- Lahaja ya **Delta** inaambukiza kwa kiasi kikubwa zaidi na imehusishwa na hatari kubwa ya kulazwa hospitalini.
- Watu waliopata chanjo kamili wana kiwango cha juu sana cha ulinzi dhidi ya ugonjwa mbaya unaotokana na COVID-19 lakini wanaweza kueneza kwa wengine.

Kumbuka ya kwamba bado inahitajika kuvaa maski kwenye nafasi za umma za ndani.

Kutoka Agosti 23, kila mtu wa umri 5 na zaidi katika jimbo la Washington anahitajika kuvaa kifaa cha kufunika uso katika nafsi za umma za ndani, kama duka ya vyakula, maduka makubwa, pahala pa mazoezi na vituo vya jamii.

Kila mtu lazima pia aendelee kuvaa maski inayotosha vizuri kwenye vituo vya marekebisho, makao ya wasio na makazi, shule, mipangilio ya kutunza watoto, usafiri wa umma na mipangilio ya huduma za afya kama vile ofisi za daktari, utunzaji wa muda mrefu na hospitali.



Kwa habari zaidi tembelea

kingcounty.gov/maski

Public Health
Seattle & King County

